## UTANGULIZI

Kilimo shadidi cha mpunga (*System of Rice Intensification—SRI*) ni teknolojia bora yenye kutumia maji na mbegu kidogo kwa kutoa mavuno mengi. Hutumika kwa kubadilishana kati ya kulowanisha kwa siku 3 na kukausha ardhi kwa siku 7 kwa kina cha sentimita 2 za maji yaliyotuama. Muda wa ukavu huweza kuwa kati ya siku 4 - 7. Mipasuko ya udongo kwenye jaruba ni kiashiria cha kumwagilia maji kwenye jaruba. Kama udongo ni wa mfinyanzi tahadhari kubwa yatakiwa kutoruhusu mipasuko ya kupitiliza kabla ya kumwagilia ili kuepuka maji mengi kupotea isivyotarajiwa.

## Kanuni bora za kilimo shadidi cha mpunga

- Tengeneza mfereji wa kuingiza na kutolea maji kwenye majaruba
- Ingiza maji ya kutosha kwenye jaruba
- Sawazisha vizuri jaruba
- Mwagilia maji kwenye kitalu na kuchukua miche ikiwa na udongo
- Pandikiza miche michanga ya umri wa siku 8 hadi 12 baada ya mbegu kuota.
- Pandikiza mche mmoja kwa kila shimo kwa kina cha sentimita 1 - 2 ardhini na muda kutoka kwenye kitalu hadi kupandikiza mche usizidi dakika 30.
- Upandaji: mche hadi mche sentimita 25, msitari hadi msitari sentimita 25.
- Udongo wa shamba usiwe na magadi
- Tumia mbolea za asili yaani samadi/ mboji. Pale ambapo samadi haipatikani tumia mbolea za viwandani .
- Mavuno mengi kwa eneo kwa maji kidogo

## Faida za Kilimo Shadidi cha Mpunga

- Kinapunguza matumizi ya maji.
- Hupunguza matumizi ya mbegu kwa asilimia 80 – 90 yaani kilogramu 5-10/ hekta moja au kilogramu 2-4/ekari ukilinganisha na kilogramu 100/hekta kwa kilimo cha kawaida.
- Hupunguza kero ya ugomvi wa maji mara kwa mara kwenye skimu za umwagiliaji.
- Mizizi ya mpunga hupata hewa ya kutosha na kuruhusu ukuaji bora wa haraka.
- Upachaji wa machipukizi mengi (98 - 118). unaotoa mavuno mengi (tani 8-12 kwa hekta).

## Mafanikio ya Kilimo Shadidi yanategemea

- Upatikanaji wa maji ya uhakika - mito, maziwa, bwawa
- Miundombinu bora ya umwagiliaji
- Asasi nzuri ya uongozi
- Mafunzo
- Nguvukazi
- Ushirikiano katika shughuli za shamba
- Upatikanaji wa pembejeo kwa wakati

## Matumizi ya mche mchanga

- Umri mdogo una uwezo wa kutoa machipukizi mengi kirahisi. (Picha Na. 1)
- Mizizi yake hukua haraka na kuweza kufyonza virutubisho vingi na hivyo mmea kutoa mavuno mengi



**Picha Na1: Mche wa mpunga wenye umri mdogo (siku 8)**

**Upandaji wa mbalimbali**

- Umbali wa sentimita 25x25 na kwa mraba
- Shamba lichavangwe na kusawazishwa vema
- Tengeneza mistari ya mraba kwa kamba, mbao iliyopigwa misumari au fremu ya chuma (Picha Na.2)

Pandikiza mche mmoja kwa shina kwa uangalifu badala ya miche 3-4 kwani hupunguza uwezo wa kugombania maji, virutubisho na mwan



**Picha Na 2: Kupiga mistari kwa kutumia fremu iliyopigiwa misumari.**

- ga

**Udhibiti wa magugu**

- Palilia kwa kutumia vifaa/mashine ya kupalilia (Picha ), madawa (viuagugu/ viatilifu).
- Matumizi ya mashine yanafaa zaidi kwa kilimo hiki



**Picha Na. 3: Mashine ya kupalilia**




*Kwa maelezo zaidi wasiliana na:*

**MKURUGENZI MKUU**
**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**
**S.L.P. 146**
**DODOMA**

*e-mail:* **info@nirc.go.tz**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

# KILIMO SHADIDI CHA MPUNGA